

NENO LA SHUKURANI KUTOKA KWA MHE. JUMA HASSAN FIMBO, MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI YA WIZARA YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE KATIKA HAFLA YA KUSAINI MKATABA WA UKAMILISHAJI WA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA ABIRIA KATIKA KIWANJA CHA NDEGE CHA MWANZA, TAREHE 28 MACHI, 2024.

Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi,

Mheshimiwa Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza,

Ndg. Michael Lushinge Masanja, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mwanza,

Viongozi wote Mliopo,

Ndugu Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mheshimiwa Waziri,

Kwa niaba ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na hadhira iliyokusanyika mahala hapa, ninapenda kukushukuru sana kwa kuwa Mgeni Rasmi wa hafla hii muhimu ya Utiaji saini Mkataba wa Ukamilishaji wa Jengo la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa heshima na taadhima, ninaomba pia nitumie fursa hii

kuzipokea na kukushukuru sana kwa pongezi nyingi ulizotupatia kwa ufanikishaji mzuri wa majukumu yetu ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Serikali nchini.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa niaba ya Menejimenti ya TAA, Nipende kusema kuwa tumepokea maelekezo yako na nakuahidi tutayatekeleza kwa ufanisi mkubwa. Niahidi pia, Menejimenti itaendelea kuweka jitihada kwa kuvitumia viwanja vyetu viweze kujiendesha kibiashara zaidi ili kuongeza mapato ya Taasisi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Waziri,

Kabla ya kumaliza, nikuahidi wewe na hadhira hii nzima kwamba, kama Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, tutafanya kazi kwa karibu na Mkandarasi ***Taifa Mining and Civil Limited*** kuhakikisha ujenzi wa Ukamilishaji wa Jengo hili, pamoja na usimikaji wa miundombinu na mifumo mbalimbali yote kwa mujibu wa Mkataba uliosainiwa leo.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa mara nyingine ninapenda kurudia kukushukuru wewe binafsi, Wizara ya Uchukuzi, viongozi wote na wananchi wote walioshirikiana nasi katika kushuhudia shughuli ya utiaji saini mkataba huu.

Mheshimiwa Waziri,

Mwisho, nikuombe utuwasilishie shukrani zetu za dhati kwa Rais wetu mpendwa, **Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa maono, miongozo na uwezeshaji wa kifedha vinavyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege vya Serikali, nchini.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Asanteni sana kwa kunisikiliza!